
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA KUMI NA MBILI
Desemba 2023



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewahakikishia wakazi wa mji mdogo wa Katesh walioathirika na mafuriko makubwa kuwa serikali itarejesha huduma zote za msingi za kijamii.

Rais Samia amesisitiza kuwa serikali itaendelea kufanya tathmini ya uharibifu wa mali huku akiiagiza Wizara ya Nishati kuangalia uwezekano wa upatikanaji wa umeme wa dharura baada ya miundombinu kuharibika na maafa haya ili shughuli za uopoaji zifanyike usiku na mchana.

Rais Samia ametoa kauli hiyo wakati akizungumza na wananchi na waathirika mara baada ya kutembelea maeneo yaliyoathirika na mafuriko hayo na kushuhudia hali halisi ya uharibifu wa maafa.

Aidha Rais Samia ameongeza kuwa mbali na michango mbalimbali iliyotolewa ndani ya nchi

lakini pia kumetolewa takriban Shilingi bilioni 2.5 kutoka kwa wahisani walioshiriki kwenye mkutano wa COP 28, Dubai.

Miongoni mwa maeneo aliyotembelea Rais Samia ni Hospitali ya Tumaini wilayani humo kwa ajili ya kuwajulia hali na kuwafariji majeruhi na pia shule ya Sekondari ya Katesh ambapo ndipo makazi ya muda yalipowekwa ili kuwastiri waathirika hao.

Vile vile, Rais Samia ametaka tahadhari zote za msingi zichukuliwe ili kusitokee janga jingine la mlipuko wa magonjwa hivyo kuheshimu kanuni za usafi kwani amesema majanga wakati mwengine huzua maradhi kama kipindupindu.

Hivyo Rais Samia ameielekeza Wizara ya Maji kuhakikisha huduma za maji safi na salama zinaendelea kupatikana muda wote huu hususan maeneo yaliowekwa makambi ya kustiri waathirika wa janga hilo.

Mafuriko mazito yaliotokea yamesababisha vifo vya Watanzania 76 hadi sasa, huku kaya 1,150 zikiwa zimeathirika na watu 5,600.

Pia kumekuwa na majeruhi zaidi ya 117 pamoja na uharibifu wa miundombinu ya barabara, maji na umeme.





# Serikali yatumia taarifa za Matokeo ya sensa ya Watu na Makazi kutambua waathirika Hanang.

Serikali imetumia taarifa za matokeo ya sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2022 kuthibitisha taarifa za makazi na kaya katika maeneo yaliyoathirika na mafuriko ya matope wilayani hanang.

Kauli hiyo ameitoa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya matumizi ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 kwa Viongozi na Watendaji wa Mkoa wa Ruvuma, iliyohusisha Kamati za Sensa na Wawakilishi wa Makundi Mbalimbali katika jamii leo katika ukumbi wa Njunde social hall – Halmashauri ya wilaya ya Songea Mkoani Ruvuma.

Waziri alisema, moja ya jukumu muhimu tulilokuwa nalo ni kupata taarifa ya hali ya kaya, makazi na mali katika maeneo yaliyoathirika kabla ya maafa hayo.

"hitaji hili lilipelekea timu ya wataalamu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuja na taarifa ya kitaalamu iliyoambatana na picha za satellite ambazo zilionyesha kwa uhakika hali ya kaya, makazi na mali zilizokuwepo katika maeneo hayo kwa idadi yake na maeneo zilizokuwepo.," alibainisha.

aliongeza kusema,licha ya kwamba tumetumia vyanzo vingine pia kuthibitisha baadhi ya masuala katika maeneo hayo, lakini chanzo chetu cha kwanza cha kuaminika kimekuwa ni matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Aidha alitumia fursa hiyo kuwakumbusha kuhusu maandalizi ya dira ya taifa 2050 ambapo serikali imetoa fursa kwa wananchi kutoa maoni na mapendekezo.

"niwasihi sana viongozi, watendaji na wananchi wote mshiriki katika zoezi hili ambalo ni muhimu kwa mustakabali mwema wa maendeleo ya nchi yetu. moja ya nyenzo muhimu zinazoweza kutuongoza kutoa maoni yetu ipasavyo historia ya taifa letu katika nyanja zote za siasa, "uchumu, jamii pamoja na kuzingatia takwimu zinazozalishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikiwemo ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022,"alifafanua.

Kwa upande wake Mwantumu Athumani Meneja Takwimu Mkoa wa Ruvuma akizungumza kwa niaba ya Mtwakwimu Mkuu wa serikali, alisema utoaji wa matokeo ya sensa ni tofauti na matukio mengine ya kitakwimu kwa kuwa wigo wa sensa ni mpana zaidi.

"Matokeo ya sensa hutolewa awamu kwa awamu kulingana na ratiba ya utoaji na usambazaji wa matokeo," alisema

Ameongeza kusema kama kuna mdau anahitaji matokeo ya sensa, ambayo hayapo kwenye ripoti zetu kwa sasa anakaribishwa kuleta maombi yake kwenye ofisi zetu za mikoa.

Naye Mkazi wa Peramiho Bw. Tito Sowela alisema elimu ya sensa ya watu na makazi imeongeza uelewa mpana wa wananchi hasa juu ya taarifa zinazokusanywa na namna zinavyoweza kusaidia serikali.

# Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, waaswa kufanya kazi kwa kushirikiana



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama ametoa wito kwa watumishi walio chini yake kufanya kazi kwa kutegemeana na kushirikiana bila kutengeneza makundi .

Ametoa rai hiyo l Mkoani Morogoro wakati akifungua kikao cha Baraza la wafanyakazi la Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na uratibu kilicholenga kujadili Taarifa ya Bajeti ya 2023-2024 ya Ofisi hiyo.

Waziri Mhagama alisema, Kuna kila sababu ya kufanya maamuzi ya pamoja ya ushirikishwaji ili kuweza kupata mafanikio kwenye idara na vitengo, kama viongozi wenu wanavyofanya kazi vizuri kwa kushirikiana.

Aliendelea kusema kuwa hata kama inafikia wakati Mtendaji hayupo kwenye Idara au kitengo kuwe kuna Mtu anayeweza kufanya kazi kwa viwango na uwezo huo huo ili mambo yaweze kwenda vizuri.

“Tukifanya kazi kwa umoja na ushirikiano tukifanikiwa tuwe tumefanikiwa wote na tukianguka tujue tumeanguka wote na tujipange ili kujua sababu ya kuanguka na tuweze kujipanga." Alibainisha.

Aidha, Waziri Mhagama alisema anafarijika na utendaji wa kitaasisi na kuwaomba watumishi kuendelea kuimarisha utendaji wa kitaasisi ambao unatoa fursa kwa kila mtu kuwa ni sehemu ya mafanikio na ufanisi wa taasisi.

“Wale ambao Mnamadaraka kwenye Idara Vitengo au Taasisi zetu Muhakikishe Mnajenga moyo wa kukuza watumishi walio chini yenu, kwa kuwapa fursa ya kukua kielimu ndani ya ofisi, kukua kiujuzi na kukua kiubobezi." Alihimiza.

Alibainisha kuwa Watumishi wa umma ni rasilimali muhimu, ya kuendesha rasilimali nyingine na kusema kuwa ni lazima tuiratibu vizuri Rasilimali hiyi na kuilinda kwa nguvu zote ili kuweza kupata mafanikio tuliyoyakusudia.

Waziri alisema; Rais wa awamu ya tatu Mhe. Benjamini Mkapa aliwahi kusema,” jambo muhimu kwa mfanyakazi si muda anaotumia kufanya kazi,bali kiasi cha kazi anachoweza kufanya katika muda aliopewa."

Alisema Kuna kila sababu ya kuanzaa kujipima wenyewe hasa katika kuelekea kuanza mwaka 2024, ili kujua kiasi cha kazi tuliyoifanya na ufanisi wake kila siku anayoshiriki kama mtumishi wa umma katika ofisi ya waziri Mkuu.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi, amesema vikao vya wafanyakazi ni tamko la kisheria ambalo chimbuko lake ni Hayati Baba wa Taifa mwalimu Julius Nyerere, Rais wa awamu ya Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilolitoa katika tamko no 1 la mwaka 1970 linalohimiza ushirikishwaji kupitia Baraza la wafanyakazi.

"Baraza ni kiungo muhimu kati ya wafanyakazi na Menejimenti na Ofisi ya Waziri Mkuu, tutaendele kuwa vikao hivi vya baraza la wafanyakazi kwa mujibu ya miongozo.

Awali akitoa salamu Katibu wa TUGHE Mkoa wa Dodoma Bw. Samwel Nyungwa ameipongeza Menejimenti ya Ofisi ya Maziri Mkuu, kwa kutekele za Sera ya ushirikishwaji kikamilifu,

Chama cha wafanyakazi kinaamini hakuna haki bila wajibu, tunaangalia namna tunavyopata haki na namna ambavyo tunatekeleza wajibu katika kuhakikisha mipango iliyopangwa inakamilika sawasawa.




# Serikali yawafuta machozi wana Mbarali Mkoani Mbeya

Serikali imekabidhi misaada ya kibinadamu yenye thamani ya shilingi Milioni 23 kwa waathirika wa maafa ya mvua iliyombatana na upepo mkali iliyosababisha kifo cha mtu mmoja, nyumba 42 kuezuliwa nyumba tatu zikibomoka kuta katika Kata sita jumla waathirika wakiwa ni 198 katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya.

Akizungumza wakati akikabidhi misaada hiyo Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa Ummy Nderiananga amesema hatua hiyo ni sehemu ya pole za Serikali kwa wananchi na kuunga mkono juhudi zilizofanyika za kukabiliana na kurejesha hali baada ya maafa kutokea ambapo amekabidhi mabati 500, Magodoro 100, na mifuko ya Saruji 200 kwa ajili ya waathirika wa maafa hayo.

Mhe. Ummy ametoa wito kwa wananchi wote kuhakikisha wanatekeleza maelekezo yote yanayotolewa na mamlaka husika ikiwa ni pamoja na kuhama katika maeneo hatarishi na kutekeleza

shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo salama akisema Kata sita zimeathirika ambazo ni I A G U R U S I , Luhanga,Ruiwa,Mawindi,Mahongol e,na Chimala.

"Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha wananchi wanaopatwa na maafa mbalimbali wanapata huduma stahiki kama ambavyo mmeona namna ambavyo Serikali inaendelea kushughulikia maafa yaliyototea Hanang na yaliyotokea hapa Mbarali na maeneo mangine kote nchini,"Amesema Mhe. Ummy.

Aidha amemuagiza Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Uongozi wa Wilaya ya Mbarali kuhakikisha unahamasisha wananchi kupanda miti kwa wingi katika maeneo yao hatua itakayosaidia kupatikana kwa hali ya hewa safi na kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza.

"Nikupongeze wewe binafsi na Kamati za Usimamizi wa Maafa Mkoa wa Mbeya kwa jitihada ambazo zimefanyika baada ya maafa haya kwa kuhakikisha wananchi wanapatiwa msaada stahiki kwa wakati pamoja na jitihada za kurejesha hali ambazo zimefanyika na zinaendelea kufanyika,"Amebainisha Mhe. Ummy.

Akitoa taarifa ya maafa Mratibu wa Maafa Wilaya ya Mbarali Bw. Lihuwi Ngonyan ameeleza kwamba mtu mmoja alithibitishwa kufariki dunia kutokana na mvua katika Kata ya Luhanga Kijiji cha Luhanga, nyumba zilizoezuliwa mapaa zikiwa ni 42 wakati zilizobomolewa kuta zikiwa ni nyumba tatu na Kaya 44 pamoja na waathirika 198 huku akiishukuru Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa msaada uliotolewa kwa waathirika hao.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mbeya Mjini Bw. Beho Malisa akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Juma Homera ameishukuru Serikali kwa msaada huo akisema ni nia njema ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wake wanaishi katika mazingira salama



# Timu ya Makatibu Wakuu yaendelea na kazi ya kuhakikisha urejeshaji wa hali Hanang unakamili

Timu ya Makatibu Wakuu wa kisekta wametembelea na kukagua zoezi la ugawaji wa misaada ya kibinandamu ikiwemo vyakula kwa waathirika wa Maafa ya Maporomoko wa mawe na tope kutoka mlima Hanang pamoja na kukagua maeneo yaliyopata athari na zoezi la kurejesha hali ikiwemo miundombinu ya Barabara na zoezi la kuondoa tope katika maeneo yaliyoathiriwa na maafa.

Ziara hiyo iliongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi amesema kuwa, Serikali imeendelea na zoezi la kurejesha hali pamoja na ugawaji wa vyakula kwa waathirika wote wa maafa hayo huku hali ya kurejesha miundombinu ya barabara na kusafisha maeneo yaliyopata athari ikiendelea.

Akizungumza kuhusu zoezi la ugawaji wa vyakula kwa waathirika hao ameeleza kuwa, Serikali itahakikisha kila aliyepaswa kupata msaada anapata kwa wakati na kwa mgawanyo sawa na miongozo iliyopo na kueleza kuwa hakuna mtu atakayekosa chakula katika mgao huo.

"Serikali imeendelea na hatua za kurejesha hali kwa wakazi wa Hanang, na hapa ujenzi wa mitaro unaendelea na utoaji wa tope zilizobaki, zoezi linaendelea vizuri na hadi sasa ni nyumba chache zimesalia kuondolewa tope," Alisema Dkt. Yonazi

Aidha alisema kuwa Wananchi waendelee kuwa na utulivu kwa kuzingatia namna Serikali inavyoendelea kuratibu lengo ni kuhakikisha wanapata misaada kama iliyokusudiwa.

"Hadi sasa watu zaidi ya 186 ndiyo waliobakia katika zoezi hilo kati ya watu1491 ambao walitakiwa kupata chakula, hivyo wote watapata chakula hakuna atakayekosa chakula, wapo waliopata awamu ya kwanza na sasa wanapewa awamu ya pili

Akizungumza kwa niaba ya wakazi wa Gendabi waliopatiwa misaada ya vyakula Bi. Stella Lili ameishukuru Serikali namna ilivyoratibu zoezi la ugawaji wa vyakula na kusema hatua hiyo imewapa Faraja na kuonesha namna Viongozi wetu wanavyowajali.

"Tunashukuru tumepewa vyakula ikiwemo Mahindi, Mchele, unga wa sembe, unga wa ngano, mafuta, chumvi, maji ya kunywa Pamoja na mahitaji mengine muhimu hakika kwa hatua hii ninaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa namna ilivyoshughulikia maafa haya," alisema Stella.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz